TANGAZO LA SERIKALI NA. 462 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) HALMASHAURI YA WILAYA YA MAFIA YA MWAKA, 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) Halmashauri ya Wilaya ya Mafia za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mafia.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma ya kuzoa taka;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"afya" maana yake hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na wala sio tu kutokuwa na ugonjwa au ulemavu;

chakula" maana yake ni kitu kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa;

"chanzo cha maji" maana yake ni eneo lolote ambalo limetengwa kwa ajili ya kuwa chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii ikiwemo visima, mito, chemchemi, vijito, na maeneo yote yanayopatikana maji;

"choo bora" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba

la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu;

"chukizo au kero" maana yake ni kitu ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha:

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;
(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi au kuleta kinyaa;
(c) kuzaliana kwa wadudu hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mafia;

"kaya" maana yake mtu mzima anayejitegemea mwanamke au mwanaume, na mtoto au watoto inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye eneo la Halmashauri;

"kelele" maana yake ni kero isababishwayo na sauti ambayo kwa asili inakataliwa au ile ambayo inaweza kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu au mazingira;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"kizimba cha taka" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuhifadhi taka ngumu;

"kituo cha maji machafu" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengenezwa kwa ajili ya ukaguzi wa mfereji ambao una mfuniko usioruhusu hewa kutoka;

"kuchakata taka" maana yake ni kuzichambua, kuzitenganisha na kuzibadili kuwa kitu kingine chenye manufaa kwa jamii;

"mabwawa ya maji taka" maana yake ni mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na

kutakasa maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, kutoka vyooni, kutoka bafuni, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zozote za nyumbani na viwanda;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya mamlaka ya Halmashauri na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

Sura 191

"maji taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191

"taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191

"taka ngumu" Maana yake ni ile iliyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara kuhakikisha kwamba-

(a) mazingira yanayozunguka eneo lake yanakuwa safi wakati wote;
(b) taka zote zinakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;
(c) anachimba shimo la kutupia taka litakalokuwa na urefu usiopungua kimo cha futi 3 na upana usiopungua futi 2;
(d) anajenga choo imara cha kudumu kilichojengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati, tembe, majani, vigae chenye mlango unaofunga na kufunguka na kuhakikisha kwamba choo kinatumika wakati wote na kuwe na chombo cha maji tiririka na sabuni ya kunawa mikono;
(e) eneo lake halina mazalia ya mbu, panya na wadudu wengine hatarishi.

Uhifadhi wa maji taka

5. Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara atatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa analo karo la kuhifadhi maji taka;
(b) kunyonya maji taka pale karo linapojaa; na

(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhia maji taka.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

6. Mtu anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa kutimiza masharti na kanuni za afya zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria na Sheria Ndogo hizi.

Ada ya ukaguzi wa kiafya

7. Kutakuwa na ada ya ukaguzi wa kiafya na italipwa na mmiliki au mhudumu katika majengo ya biashara, vituo vya afya na zahanati za watu binafsi, famasi au maduka ya madawa, hoteli, migahawa, mama au baba lishe, watoa tiba asili, majengo ya biashara na vioski (*groceries*) na maeneo mengine kama ilivyoainishwa katika katika Jedwali la Kwanza.

Upimaji wa afya

8. Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, nyumba za kulala wageni, bucha, waoka mikate, au watu wanaoshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa kuhakikisha kwamba wanapima afya zao kila baada ya miezi sita.

Ada ya kuzoai taka

9.-(1) Kutakuwa na ada ya uzoaji taka ambayo itatozwa na Halmashauri kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa mazingira kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili.

(2) Ada ya uzoaji taka italipwa tarehe ishirini na nane ya kila mwezi na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya kieletroniki na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(3) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo, Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Mamlaka ya Afisa

10. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya-

(a) kuingia katika eneo lolote ndani ya

Mwidhiniwa

Halmashauri kuanzia saa moja kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; na

(b) kushauri au kuelekeza watu au mtu kutokuishi katika jengo ambalo linahatarisha afya au maisha ya watu na viumbe hai.

Vifaa vya kuhifadhi taka ngumu

11.-(1) Kila mmliki wa jengo la makazi au mpangaji wa jengo la makazi au mtu yeyote anayefanyia biashara katika eneo lolote ndani ya Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhia taka chenye mfuniko na atawajibika kukusanya taka hizo kwenye vizimba vya kuzolea taka katika maeneo yaliyoainishwa.

(2) Kila mmiliki wa jengo au mpangaji wa nyumba iliyoko katika ukanda wa kijani, katika maeneo ambayo hayajapimwa atalazimika kuwa na shimo kubwa la kukusanyia taka ngumu katika eneo lake.

Ukusanyaji taka ngumu

12.-(1) Halmashauri itawajibika kukusanya taka ngumu kutoka katika vizimba vya taka vilivyoainishwa katika kila kata.

(2) Taka ngumu zote zitakazokusanywa kwenye mapipa ya taka zitabaki kuwa mali ya mkazi au mmliki wa eneo lile mpaka zitakapokuwa zimefikishwa kwenye kizimba cha taka au zitakapokuwa zimetolewa na Wakala kutoka katika eneo lake.

(3) Haitaruhusiwa kwa mtu yeyote-

(a) kuweka uchafu wenye asili ya maji maji kwenye pipa la taka au kitu chochote kinachoweza kulipuka na kusababisha madhara; na

(b) kuchoma au kufukia taka ngumu bila kibali cha Halmashauri.

Eneo la kutupa taka

13. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka;

(b) kuweka vyombo maalum vya kutunzia taka; na

(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo

kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

Udhibiti utupaji wa taka

14.-(1) Watumiaji wa vyombo vya usafiri binafsi au vya umma hawataruhusiwa kutupa taka nje ya vyombo hivyo, na taka zote zitatakiwa kuwekwa kwenye chombo cha kuhifadhia taka kilichomo kwenye chombo husika.

(2) Mtu hataruhusiwa kutupa taka ovyo katika maeneo ya makazi, biashara, mifereji ya maji ya mvua, hifadhi ya barabara au mahali popote ambapo si rasmi kwa ajili ya kutupa taka.

(3) Mtu au mkazi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.

Udhibiti wa kelele kupita kiasi

15. Mtu hataruhusiwi kusababisha au kufungulia kwa kelele kupita kiasi iwe muziki, kelele za kiwanda, jenereta au kitu kingine chochote (*sound pollution*) bila kupata kibali cha Afisa Mwidhiniwa.

Kutiririsha maji taka

16.-(1) Mtu hataruhusiwa kutiririsha au kumwaga au kuruhusu au kusababisha kutiririsha au kumwaga maji taka barabarani, uchochoroni kwenye mifereji, mtoni, kwenye vyanzo vya maji au sehemu yoyote ambayo si rasmi kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

(2) Kila kiwanda kinachozalisha maji taka kitakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kinaunganisha maji taka au kujenga mifereji na mabwawa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

(3) Kila mmiliki wa nyumba atatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo hilo linapojaa; na

(b) itakuwa ni marufuku kwa mtu kuacha karo kujaa na kutiririsha maji taka barabarani au sehemu yoyote isiyoruhusiwa.

Utengenezaji na uuzaji vyakula

17.-(1) Mtu hataruhusiwa kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha na kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba yoyote mpaka awe

ametimiza masharti na kanuni za afya yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

(2) Kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia nzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

Uzuiaji wa shughuli wakati wa magonjwa ya mlipuko

18. Mkurugenzi anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wakati wa zuio

19.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kumkamata mtu yeyote ambaye atakaidi amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo mtu aliyekamatwa alikuwa anauza vyakula ambavyo vinaharibika kwa haraka, Halmashauri itaharibu vyakula hivyo.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) na (2), iwapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka, Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.

Wajibu wa mfanyabiashara wa bucha na maduka ya nyama

20. Kila mfanyabiashara wa bucha au duka la nyama atatakiwa kuhakikisha kuwa-

(a) ana leseni na vibali vya kufanya biashara hiyo;
(b) kuna kabati la vioo la kuzuia nzi na wadudu wengine wataambao;
(c) kuna pipa la kuhifadhia taka ngumu na laini;
(d) kuna jokofu la kuhifadhia nyama;
(e) jengo lake la biashara lina mwanga wa

kutosha, umeme, maji safi na salama, visu, meza, mzani wa kawaida au mzani wa kielektroniki, na misumeno maalumu ya kukatia nyama;

(f) nyama imekaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa na kugongwa muhuri na inauzwa ndani ya jengo;

(g) muuzaji anavaa sare nyeupe muda wote ambazo ni mabuti, koti na kofia; na

(h) biashara ya nyama inafanyika katika bucha na maduka maalum na si vinginevyo.

Siku ya usafi

21.-(1) Kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi itakuwa ni siku maalam ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi na umma.

(2) Itakuwa ni wajibu na lazima kwa kila mkazi katika kijiji na kitongoji kushiriki usafi wa mazingira kwa siku iliyopangwa na Halmashauri katika maeneo yao na maeneo ya umma.

(3) Kila mtu atahakikisha eneo la makazi yake na vichochoro vilivyomzunguka, eneo analofanyia biashara, eneo la wazi lililokaribu naye kwa umbali wa mita kumi na eneo la mazingira ya ofisi ni safi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

22.-(1) Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba-

(a) nyumba yake ina choo safi, imara kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo;

(b) anaweka sehemu maalum ya kunawia mikono ikiwa na maji safi na sabuni maalum ya kimiminika.

(2) Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka chanzo chochote cha maji.

Vyoo vya umma

23.-(1) Halmashauri inaweza kujenga choo cha umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya Umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa.

(2) Vyoo vitakavyojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitatakiwa viwe vya kudumu na-

(a) vyenye matundu yasiyopungua mawili (2) kwa wanawake na mawili (2) kwa wanaume;
(b) vyenye mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama;
(c) kuwepo na chombo cha kuhifadhia maji ya akiba;
(d) kuwepo kwa bafu ya wanaume na wanawake;
(e) kuwepo na chumba maalum cha kuvutia sigara;
(f) kuwepo na sehemu ya haja ndogo kwa wanaume; na
(g) kuwepo na chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji;

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

24. Ni wajibu wa mtu yeyote, kikundi au taasisi yoyote yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano au sherehe au mkusanyiko wowote, kuweka au kujenga vyoo vya muda endapo eneo hilo hakuna vyoo vya kudumu na atatakiwa kuomba idhini kutoka Halmashauri.

Ilani ya kujenga au kurekebisha choo

25. Afisa Mwidhiniwa atafanya ukaguzi wa afya na iwapo katika ukaguzi huo itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu.

Ilani ya kuondoa kero

26.-(1) Katika ukaguzi afya, Afisa Mwidhiniwa akigundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ndani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika, akimtaka kuondoa kero hiyo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne.

(2) Mtu atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa anatenda kosa.

Vikundi vya

27. Halmashauri itahamasisha uundaji wa ikundi

usafi

Jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa, baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Wajibu wa mfugaji

28. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi atatakiwa-

(a) kupitisha mfugo au mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;
(b) kufuga na kulisha mifugo katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;
(c) kuwa na kadi ya mfugo au mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
(d) kuchangia gharama za ukarabati wa josho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;
(e) kupeleka mfugo au mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;
(f) kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;
(g) kuweka alama kwenye mfugo au mifugo yake na katika viungo vya mfugo au mifugo vinavyopendekezwa na mamlaka husika ili kutoharibu zao la ngozi;
(h) kupeleka mfugo au mifugo katika josho kama atakavyoagizwa na Halmashauri.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

29.-(1) Halmashauri itakamata mfugo au mifugo yoyote itakayoonekana inazurura ovyo katika eneo la Halmashauri.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa mahali pasipostahili utatozwa faini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tano.

(3) Endapo mfugo uliokamatwa hautachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba (7) tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo huo baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmliki wa

mfugo huo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mfugo, gharama ya Mahakama na gharama ya mnada.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (3), Halmashauri kabla ya kuuza mfugo huo kwa mnada, itamjulisha mmliki na umma juu ya kusudio hilo.

(5) Endapo kutatokea kufa kwa mfugo au mifugo kutokana na sababu yoyote ile, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama vifo hivyo vimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Marufuku

30. Ni marufuku-

(a) kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upulizaji dawa au biashara ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni kutoka Halmashauri;

(b) kwa mfanyabiashara yeyote kupanga bidhaa nje ya jengo lake la biashara au barabarani au vichochoroni au katika eneo lolote ambalo halikuidhinishwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(c) kwa mtu yeyote kutupa taka za aina yoyote barabarani au eneo lolote la wazi au kwenye vichochoro au kwenye chanzo chochote cha maji au katika eneo lolote ambalo halikutengwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(d) kwa mtu yeyote aliye ndani ya gari kudondosha taka ngumu nje ya gari likiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ile ambapo gari hilo linapita;

(e) kwa mtu yeyote kuweka kitu chochote kwenye maji taka ambacho kinaweza kuathiri mtu yeyote au kuharibu mfumo wa tiba ya maji taka au kinachoweza kusababisha kuzuia mtiririko wa maji taka;

(f) kwa mtu yeyote kulima kilimo cha matuta yanayosababisha maji kutuama ndani ya eneo la katikati ya mji;

(g) kuchimba mchanga au kokoto au mawe katika

vyanzo vya maji au mito barabarani;

(h) kuchafua au kuoga au kufulia au kuvuruga maji yanayotumika kwa ajili ya matumizi ya binadamu au wanyama;

(i) kuuza mchanga au kokoto na mawe kandokando mwa barabara;

(j) kufanya biashara ya pombe ya aina yoyote katika nyumba au kwenye maeneo ya akiba za barabara au mitaani;

(k) kuuza matunda au bidhaa nyingine za vyakula barabarani au kuanzisha masoko au magenge ya kuuzia matunda au vyakula au biashara nyingine ndogo bila ruhusa ya Halmashauri;

(l) kuunganisha bomba la taka vimiminika katika mifereji ya maji ya mvua;

(m) kufungulia au kutiririsha maji ya choo au taka vimiminika katika mkondo asili wa maji ya mvua au barabara au mfereji wa barabara wa maji ya mvua;

(n) kujisaidia haja ndogo au haja kubwa barabarani au mitaani au sehemu yoyote isiyokusudiwa kwa madhumuni hayo;

(o) kufanya mikusanyiko ya kidini au kiutamaduni au kijamii wakati wa milipuko ya magonjwa ya kuambukiza, isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Halmashauri na usimamizi wa Afisa Afya; na

(p) kuweka uchafu wenye asili ya maji maji kwenye pipa la taka au kitu chochote kinachoweza kulipuka na kusababisha madhara.

Makosa

31. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote-

(a) kujenga choo chini ya umbali wa mita 60 kutoka kisimani, bwawani, mtoni, au chanzo kingine cha maji yanayotumika, kwa matumizi ya binadamu;

(b) kutoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, maji machafu, yenye kinyesi kutoka kwenye choo chake au bafu lake au karo la kuoshea

vyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua maji machafu na kuyatitirisha kwenye barabara, mitaa, au kwenye mifereji ya maji ya mvua, au mfereji wowote uliowazi;

(c) kutupa taka au kusababisha mtu mwingine atupe taka mahali popote pasiporuhusiwa na Halmashauri;

(d) kutolipa ada ya taka kwa miezi miwili mfululizo;

(e) kutembeza vyakula mitaani bila kibali cha Halmashauri;

(f) kutokuwa na pipa la taka lenye mfuniko katika eneo la biashara;

(g) kutokuwa na choo au kukutwa na choo kibovu au kilichojaa;

(h) kukutwa na shimo la maji taka lililojaa au ambalo halina mfuniko;

(i) kutokuwa na chombo maalum cha kukusanyia taka ndani ya gari la abiria; na

(j) atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo si rasmi kwa kufanya shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri;

Adhabu

32. Mtu atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili, au vyote kwa pamoja.

Ufifilishaji wa makosa

33. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa lililoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 158 cha Sheria, iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Sita na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

## JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7*)

ADA YA UKAGUZI WA AFYA

| NA. | AINA YA BIASHARA | ADA KWA MWAKA (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Baa na maduka ya vinywaji (groceries), bucha | 5,000/= |
| 2 | Migahawa na mama lishe | 2,000/= |
| 3 | Nyumba za wageni (Guest House) na hoteli | 10,000/= |
| 4 | Kumbi za starehe au mikutano | 10,000/= |
| 5 | Ukaguzi wa mitambo, maeneo ya madini ikiwemo ya ujenzi | 30,000/= |
| 6 | Majengo mengine ya biashara | 7,000/= |
| 7 | Viwanda vikubwa | 100,000/= |
| | Viwanda vidogo | 20,000/= |
| 8 | Hoteli za kitalii | 100,000/= |

JEDWALI LA PILI

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9(1)*)

ADA YA UZOAJI TAKA KATIKA MAJENGO NA MAENEO MENGINE

| NA. | ENEO | ADA KWA MWEZI (TZS) |
|---|---|---|
| 1. | Kaya moja | 1,000/= |
| 2. | Maduka la rejareja | 3,000/= |
| 3. | Mashine ya kukamua mauta ya nazi | 5,000/= |
| 4. | Maduka la jumla | 5,000/= |
| 5. | Migahawa (Restaurant) | 3,000/= |
| 6. | Mashine za kukoboa/kusaga | 5,000/= |
| 7. | Vilabu vya pombe za kienyeji, baa, grocery | 5,000/= |
| 8. | Mama lishe/Baba lishe, nyama choma/chipsi inayojitegemea | 3,000/= |
| 9. | Viwanda vidogo vya useremala na mashine za mbao, karakana na vinavyofanana na hivi. | 10,000/= |
| 10. | Bucha (maduka ya nyama, samaki) | 5,000/= |
| 11. | Nyumba za kulala wageni | 5,000/= |
| 12. | Saluni (Ususi/Vinyozi) | 3,000/= |
| 13. | Gereji | 10,000/= |
| 14. | Godown (Ghala) | 7,000/= |
| 15. | Kituo cha kuuza mafuta (Filling station) | 10,000/= |
| 16. | Ofisi za Taasisi mbalimbali | 10,000/= |
| 17. | Hoteli | 10,000/= |
| 18. | Stoo za mkaa | 5,000/= |
| 19. | Mafundi kushona nguo | 2,000/= |
| 20. | Meli/vivuko | 100,000/= (kwa mwaka) |
| 21. | Kumbi za starehe, sinema | 10,000/= |
| 22. | Majengo/maeneo ya kuoshea magari/pikipiki | 5,000/= |
| 23. | Zahanati/kituo cha afya au hospitali | 20,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 24. | Majengo mengine yasiyotajwa | 20,000/= |
| 25. | Wakandarasi | 50,000/= (kwa mwaka) |
| 26. | Maeneo yanayochimbwa madini mfano mchanga na vifusi | 5,000/= |
| 27. | Viwanda vikubwa | 10,000/= |

JEDWALI LA TATU

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 25*)

ILANI YA KUJENGA CHOO

AYA YA I

Ndugu ……………………….……simu………………..wa Kitongoji cha ……………………………….Kijiji………………..Kata……………………….. Tarafa ……………………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika tarehe …………………mwezi……………..mwaka……………katika nyumba yako ya biashara/kuishi/kutolea huduma/Namba iliyopo eneo la …………………….katika Kitongoji/Mtaa*………….……….Kijiji cha …………….………Kata ya …………………. Imekuwa haina choo/choo kimejaa/kimeharibiwa*, hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo: -

1. …………………………………………………………………………
2. …………………………………………………………………………
3. …………………………………………………………………………
4. …………………………………………………………………………

AYA YA II

Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika aya ya I ya ilani hii.

AYA YA III

Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe ……………. Endapo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

Saini ……………………………………………

Majina……………………………………….

Simu……………………………………………

Aya hii mtu aliyekosa kama amepatikana wakati wa kutoa ilani.

SHAHIDI ALIYETHIBITISHA NI: IMETOLEWA NA:

Saini ……………………………………….. Saini ………………………………..

Majina ……………………………………. Majina ……………………………..

Simu ……………………………………… Wadhifa ……………………………

Tarehe ……………………………………. Tarehe ……………………………..

*Futa lisilohusika

JEDWALI LA NNE

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 26(1)*)

ILANI YA KUONDOA KERO

AYA YA I

Ndugu ………………………simu…………………..wa Kitongoji cha …………………….Kijiji……………………..Kata…………….. Tarafa ………………………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika tarehe …………………mwezi……………..mwaka……………katika nyumba yako ya biashara/kuishi/kutolea huduma/Namba iliyopo eneo la …………………….katika Kitongoji/Mtaa*……………..………Kijiji cha ……………..………Kata ya …………………. Tumekuta machukizo/kero/uchafu*, hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

1. ………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………
4. ………………………………………………………………………

AYA YA II

Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha/kuondoa/kusafisha* kwa:

1. ………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………
4. ………………………………………………………………………

AYA YA III

Unapewa muda wa siku saba (7) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu ya II ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

Saini

……………………………………….Majina………………………………….simu………

Aya hii mtu aliyekosa kama amepatikana wakati wa kutoa ilani.

SHAHIDI ALIYETHIBITISHA NI:

Saini ………………………………………..Saini

Majina …………………………………….  Majina

Simu………………………………………...Simu

IMETOLEWA NA:

Wadhifa……………………………………..Wadhifa

Tarehe ………………………………………Tarehe

*Futa lisilohusika

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 29(2))*

VIWANGO VYA FAINI KWA MFUGO AU MIFUGO INAYOZURURA

| NA. | AINA YA MFUGO | KIWANGO CHA FAINI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 50,000/= kila ng'ombe |
| 2. | Punda | 40,000/= kila punda |
| 2 | Mbuzi | 30,000/= kila mbuzi |
| 3 | Kondoo | 30,000/= kila kondoo |
| 4 | Wanyama wengine | 15,000/= kila nguruwe |

JEDWALI LA SITA

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 33*)

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi;………………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya;…………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, kwamba mnamo tarehe;…… ya Mwezi;….…. Mwaka;……..… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:

Leo tarehe;…....... ya Mwezi;………… Mwaka;…………..

Jina;………………………………..…………………….

Saini;………………………..……………………………

MBELE YANGU :

Jina;…………………………..……..……………………

Wadhifa;……………………………………………..…….

Saini;…………………………………………………………

Tarehe;……………………………………………………….

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mafia imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Mafia uliofanyika tarehe 31 mwezi 05 Mwaka 2022 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya:-

KASSIM SEIF NDUMBO
*Mkugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mafia*

JUMA SALUM ALLY
*/Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Wilaya Mafia*

NAKUBALI,

/

L.S

Dodoma,

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*